

Livestock and Fisheries minister Abdallah Ulega (2nd-R, gesturing) shows members of an Egyptian delegation now visiting Tanzania the type of cattle bred at the Kongwa Ranch in Kongwa District, Dodoma Region, on Monday. Left is the CEO of Egypt's National Fishing Company and Aquaculture Development, Islam Attia Abdel Hamid, followed by the Chairman of Egypt's Veterinary Services, Maj Gen Dr Ihab Saber Youssef. Photo: Correspondent Mbaraka Kambona

# Gov ha co in

By Co

TH Scien ann Me (Mo of tea ki

of d a t

VIPAUMBELE>> Kupunguza mabadili

# Wafugaji kuchangamkia fursa uuzaji nyama Misri

Na IRENE MWASOMOLA

CHAMA cha Wafugaji Tanzania (CCWT), kimesema kitatumia ipasavyo fursa ya uuzaji nyama nchini Misri, kwa kuwa na malisho na mbegu bora.

Pia, kimesema kitahakikisha kinafuga kisasa na kuzalisha mifugo inayokidhi soko la kimataifa.

Katibu wa CCWT, Joshua Lugaso, alisema hayo alipozungumza na gazeti hili jana ikiwa imepita siku moja tangu serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Huduma za Miradi nchini Misri (NSPO), kukubaliana kuanza kuuza nyama ya Tanzania, nchini Misri na kuwa kabla ya sikukuu ya Eid al Hajj tani 100 zitasafirishwa.

Lugaso, alishukuru serikali kwa

> **Viongozi waliotoka Misri wamekuja kufunga mikataba na kampuni za hapa nyumbani, wamekwenda na jopo la madaktari kukagua baadhi ya machinjio zetu...**
>
> Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega.

kufungua fursa hiyo ya kibiashara na jitihada mbalimbali inazofanya kukuza sekta ya ufugaji nchini.

Alisema kutokana na fursa hiyo, watahakikisha wanawapatia ng'ombe malisho bora kwa lengo la kuzalisha nyama yenye viwango.

Lugaso alimshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyofungua nchi na kuvutia wawekezaji katika sekta ya mifugo.

"Tunaishukuru sana serikali yetu chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa tunaamini neema hii imetokana na matunda ya ziara zake nje ya nchi na sisi wafugaji tutahakikisha tunatumia vizuri fursa hii tutafuga kisasa, tutakuwa na mbegu bora kuzalisha mifugo yenye nyama inayokidhi viwango vya soko la kimataifa,"alisema.

Akizungumza na kituo cha redio cha Wasafi jana, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema juzi madaktari walianza kukagua baadhi ya machinjio nchini yakiwemo ya mkoani Mwanza kwa lengo la kuangalia ubora.

"Viongozi waliotoka Misri wamekuja kufunga mikataba na kampuni za hapa nyumbani, wamekwenda na jopo la madaktari kukagua baadhi ya machinjio zetu,"alisema.

Mbali na hayo, Ulega alisema pamoja na mambo mengine amezungumza na ujumbe uliotoka Misri kuhusu kutoa fursa ya kuwapa vijana mitaji ya kufanya mradi wa unenepeshaji mifugo.

Alisema ameushawishi ujumbe huo kuleta mitaji ya fedha na kuingia mikataba na vijana kwa lengo la kuendeleza biashara hiyo.

Ulega aliongeza nchi ya Misri ina mahitaji makubwa ya nyama na mifugo hai, hatua ambayo ni fursa ya biashara kwa Tanzania na kwamba fursa hiyo imetokana na ziara ya Rais Samia aliyoifanya nchini Misri.

Juzi akiwa jijini Dodoma, Waziri Ulega alifanya mazungumzo na Makamu Mwenyekiti wa Taasisi ya Huduma za Miradi nchini Misri (NSPO), Meja Jenerali Hossam Nigeda na kusema wamejipanga kuanzisha machinjio ya kisasa nchini, itakayowawezesha kusafirisha tani 600 ya nyama kila mwezi.

CHETI



CamScanner